# OFISI YA RAIS- TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO
# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA LUGALO

**Anuani ya Simu:**
**Simu Na: 0783121609 / 0758 352 855**

S.L.P 2324
**KILOLO**
IRINGA

**KUMB NA: LGSS/KDC/IRA/2024/1** **Tarehe:** 15/04/2024

**JINA LA MWANAFUNZI: ..........................................................................**

**……………………………………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA LUGALO MWAKA 2024**

---

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Lugalo kwa mwaka 2024. Shule ipo Kijiji cha Mbigili, Kata ya Lugalo, Tarafa ya Mazombe, Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa Umbali wa Kilomita 25 kutoka Manispaa ya Iringa na Kilomita moja (1) kutoka Barabara kuu ya Tanzania – Zambia upande wa Kushoto ukitokea Manispaa ya Iringa. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **01.07.2024**, unatakiwa kuripoti shuleni kabla ya saa 10 jioni. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14.07.2024** ndani ya siku (14).

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Serikali inagharamia elimu hivyo mwanafunzi atasoma bila mzazi kulipa ada isipokuwa kama kuna mchango wa fedha ambao wazazi kupitia vikao na kamati / bodi ya shule iliridhia kwa pamoja. Aidha, wajibu wa mzazi ni kununua sare za shule, Vifaa vya kujifunzia kama madaftari, kalamu, na matibabu.

## 2.1 SARE YA SHULE

a) Shati mbili (2) tetroni rangi nyeupe ya mikono mirefu.
b) Sketi mbili za rangi ya **drafti nyekundu (C – 74** A**), Zingatia namba ya kitambaa** malinda kumi. Matano mbele na matano nyuma. Sketi iwe ndefu karibu na kisigino. *(Kitambaa kimeambatanishwa)*
c) Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (2) vyenye visigino vifupi
d) Sweta zenye rangi nyekundu mbili (02)
e) Track Suit rangi ya bluu nyeusi na Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo.
f) Soksi nyeupe jozi nne (04), Tai ndefu rangi nyekundu.
g) Hijabu nyeupe mbili (02) zisizo na mapambo yeyote kwa wasichana wa kiislam.

**AINA YA KITAMBAA KWA AJILI YA KUSHONEA SKETI**




## 2.3 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI (KITAALUMA)

Mwanafunzi anapokuja kuanza kidato cha kwanza aje na mahitaji yafuatayo atakayotumia darasani.

i. Daftari kubwa za kutosha (counter books 4 quires) Zisipungue nane (8)**,** Begi la kubebea daftari**,** Rula, penseli na karamu za wino za kutosha.
ii. Mkebe (Mathematical set) 01
iii. Non – Programmable Scientific Calculator 1. *(Fx – 991MS)*
iv. Saa ya mkononi kwa ajili ya kumsaidia mwanafunzi kutunza muda isiyo **Smart Watch.**

## 2.4 MAHITAJI MENGINE YA SHULE

i. Bunda moja (01) la karatasi A4 (Duplicating Ream Paper A4) kwa muhula mmoja.
ii. Vifaa vya usafi (Water Squizer,Ufagio, Kwanja,Reki iliyonolewa na jembe lenye mpini).
iii. Ndoo 2 (kubwa na ndogo) kwa ajili ya kuhifadhia maji na kuogea.
iv. Raba jozi 1 kwa ajili ya michezo pamoja na bukta ya Rangi Nyekundu
v. T-shirt 1 ya njano ya kuvaa muda ambao siyo wa darasani na michezoni.
vi. T-shirt 1 ya Kijivu yenye nembo ya shule (Itapatikana shuleni)
vii. Gauni 2 au zaidi rangi ya Light Blue za kushindia (Shamba dress) mshono wa solo.
viii. Jozi 2 za Kitenge au Kanga na Blanket.
ix. Nguo za ndani za kutosha, Toilet paper 5.
x. Mahitaji mengine ya kutosha ya kisichana (*Taulo za kike*) si chini ya paketi 5.
xi. Mafaili mawili (*Flat Plastic Files*)
xii. Vifaa vya malazi (Godoro futi $2\frac{1}{2} \times 6$, Mashuka mawili rangi ya Pink, Mto wa kulalia mmoja (1), chandarua rangi ya Pink na blanket)
xiii. Vyombo vya chakula kama sahani, kijiko, kikombe

xiv. Taulo moja la kuogea na kandambili
xv. Sabuni za kufulia na kuogea (medicated soap) za kutosha.
xvi. Fedha za kutosha za matumizi binafsi ya mwanafunzi.
xvii. Kwa wasichana wanaovaa **Hijab** waje na za kushindia mbili rangi ya damu ya mzee
xviii. Ni lazima mwanafunzi akaja na kadi ya BIMA YA AFYA au aje na tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa matibabu ya mwaka mzima (NHIF). Kadi ya bima afya itakaguliwa au pesa itapokelewa siku ya kuripoti.
xix. Ni vema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni awe amechukua **tahadhari zote za kiafya.**
xx. Picha za wazazi au walezi *(Passport size)* kwa kila mzazi/mlezi na mwanafunzi (mbili) zibandikwe kwenye fomu iliyoambatishwa.

## 2.5 MICHANGO MUHIMU YA SHULE

| SN | MATUMIZI | KIASI | AKAUNTI NAMBA |
|---|---|---|---|
| 01 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= | **XXXXXXXXXXXX – NMB**<br>LUGALO GIRLS' PROJECT ACCOUNT<br>*Bank Pay Slip* – **BPS** |
| 02 | Tahadhari | 5,000/= | |
| 03 | Kitambulisho | 5,000/= | |
| 04 | Nembo | 5,000/= | |
| | **Jumla** | **80,000/=** | |

## 2.6 KUBADILI JINA

Hautaruhusiwa kubadili jina. Jina lako linatakiwa kuwa kama ilivyotumika wakati wa mtihani wa kidato cha nne kwenye SELF – FORM yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili. Mwanafunzi anaporipoti shuleni, anatakiwa kuja na nakala (Photocopy) ya cheti chake cha kuzaliwa na Result slip. Hii itasaidia kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa usajili wa mtihani wa taifa.

## 2.7 KUWATEMBELEA WANAFUNZI / SIKU YA WAGENI SHULENI

Wazazi/walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa muhula kwa tarehe itakayopangwa itakuwa siku ya Jumapili kuanzia saa 04.00 asubuhi mpaka 10.00 jioni. Mwalimu wa darasa atakuwepo kuonana na wazazi ili kujadiliana kuhusu maswala ya kitaaluma na nidhamu ya mwanafunzi. Hairuhusiwi kumletea mwanafunzi aina yoyote ya chakula. Aidha, mawasiliano mengine muhimu yapitie kwa Mkuu wa Shule kwa anuani iliyopo hapo juu au simu Namba +255 758 352 855 au +255 783 121 609.

**N.B:**
**Hairuhusiwi kumletea simu, line, au chaja siku hiyo, ikibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

### 2.8 MPANGO WA USAFIRI

Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli. Usafiri wa kufika Iringa ni kwa njia ya mabasi. Mwalimu wa usafiri atakusaidia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda na kurudi likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema, ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na.25 ya mwaka 1978** kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria **Namba 10 ya Mwaka 1995** na inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu, pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa masuala ya Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

a) Mahudhurio Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka kwenye Uongozi wa Shule.

i. Kuwahi kuamka na kufanya maandalizi ya asubuhi na kuwa mstarini (parade) saa 12.30 (saa kumi na mbili na nusu) asubuhi kila siku za masomo
ii. Kuhudhuria vipindi vyote kwa muda wote wa masomo kwa siku zote za wiki.
iii. Kuhudhuria kazi zote za mikono zitakazopangwa ama kujitokeza kwa dharula.
iv. Kuhudhuria mikutano ya shule, mfano; Baraza la shule,Ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, Maandamano, vikao vya madarasa, Masomo ya Dini n.k.
v. Kuitika miito ya dharula mara moja.

b) Kuwathamini na kuwaheshimu wanafunzi wenzako wote wakubwa kwa wadogo
c) Kusimama na kumsalimu Mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo na kupokea mizigo ni lazima.
d) Ni wajibu wako mwanafunzi Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, kutii kengele na kuwahi kila mahali utakapohitajiwa na kwa wakati.
e) Kutumia lugha nzuri wakati wote unapokuwa shuleni na hata nyumbani
f) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote pamoja na kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi.
h) Kuitika wito mara moja kukimbilia aliko anayekuita
i) Kuheshimu bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa vyama, serikali na Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule na fedha za Taifa.
j) Kuheshimu vikao, Ofisi za shule, mali binafsi na za umma.
k) Kukaa kimya darasani na mahala pengine popote penye mkusanyiko.
l) Kutoka nje ya darasa kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa

m) Huruhusiwi kutumia madawa ya kulevya kama pombe au sigala ndani na nje ya shule
n) Kuwa mfano mzuri wa kuigwa (kitabia) uwapo ndani na nje ya shule
o) Si ruhusa kugombana, au kutukana, au kupigana
p) Huruhusiwi kushiriki uasherati (uzinzi), Wizi na utapeli
q) Huruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum baada ya kufika shuleni.Kibali maalumu cha ruhusa kitatolewa na mwalimu wa zamu au mwalimu wa Darasa au mwalimu wa malezi. Siku za ibada wanafunzi wataambatana na walimu wao kwenda ibadani.
r) Usitembelee maeneo yafuatayo bila ruhusa toka kwa mwalimu

i. Ofisi za shule
ii. Maabara
iii. Nyumba za wafanyakazi / walimu

s) Huruhusiwi kabisa kutembelea maeneo yafuatayo ukiwa ni mwanafunzi aidha ikiwa ni muda uko shuleni au ukiwa nyumbani wakati wa likizo.

i. Vilabu vya pombe au bar (Sehemu zote zinazouza vileo)
ii. Majumba ya kufikia wageni. (Guest House/ Lodge)
iii. Majumba ya starehe kama vile majumba ya disco au klabu.
iv. Nyumba za kuoneshea mpira au kucheza michezo ya video na kamari.
v. Sehemu wanazokodisha mikanda ya video na kuingiza nyimbo kwenye simu *(Studio).*

### 3.1 UTARATIBU WA UVAAJI SARE YA SHULE

i. Unapaswa kuwa na sare ya shule zinazokubalika na kwa wakati kama utakavyopangiwa kwa:
   a) Wakati wa masomo
   b) Safari za nje ya shule kwa jina la shule
   c) Wakati wa maandamano
   d) Kuwa na Nguo za Michezo na vazi la kazi za mikono.

ii. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa viatu vyenye kisigino kirefu, soli ndefu au pana wala kiatu kilichochongoka mbele, mapambo mengine kama heleni, mikufu, bangili hayaruhusiwi. Pia ni marufuku kufuga rasta, nywele ndefu, kupaka kucha rangi, kupaka wanja, kupaka piko, kujichubua, kunyoa kipara au kiduku. Atakaye patikana na makosa haya atarudishwa nyumbani na kumwita mzazi ama kufukuzwa shule kabisa.

### 3.2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

a) Wizi
b) Utoro
c) Ulevi wa aina yeyote
d) Uvutaji au uuzaji wa bangi, sigara, mirungi, kubeli na mihadharati mingine.
e) Kosa la jinai
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g) Kuolewa
h) Kuwa na mahusiano ya kimapenzi ndani na nje ya shule.
i) Kupata mimba.
j) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea au kusababisha mgomo.
l) Uzinzi, Ushoga, usagaji, na ubakaji au ulawiti
m) Kupiga au kupigana
n) Kudharau Bendera, Nembo, fedha, Wimbo wa Taifa na Viongozi wa kitaifa
o) Kumiliki simu ya mkononi ama kifaa chochote cha simu kama charger au laini.
p) Kumiliki pasi ya umeme, Heater au vifaa vingine vinavyotumia umeme.
q) Kugomea/ kukataa adhabu kwa makusudi
r) Makosa mengine yafananayo na hayo hapo juu.

**MUHIMU:**

i. **Lugha ya mawasiliano kwa mwanafunzi awapo shuleni ni Kiingereza. Kamwe hairuhusiwi kuzungumza lugha nyingine tofauti na Kiingereza katika mazingira ya shule.**

ii. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

## 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni. ***(Imeambatanishwa)***
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

## 5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO HAYA NA KUYATEKELEZA IPASAVYO

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi na kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa aidha kwa ajili ya matibabu au vinginevyo.

***Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi au Mtoto wako usitume chochote ni vyema ukawasiliana na Uongozi wa Shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba ifuatayo:-*** **Mkuu wa Shule**: **0758 352 855 / 0783 121 609**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA SEKONDARI YA WASICHANA LUGALO**

**……………………….**
**NAJA A. MSOKWA**
**MKUU WA SHULE**
**Simu: 0758352855 / 0783121609**

**NAKALA:**

- **Katibu Mkuu, - TAMISEMI**
- **Mkurugenzi Mtendaji (W), KILOLO**

## 6.0 (a) MEDICAL EXAMINATION FORM

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**LUGALO GIRLS' SECONDARY SCHOOL**

(To be completed by a Medical Officer in respect to all form five students)

---

**STUDENT'S FULL NAME**……………………………………………………..…………………………………

Please examine the above named student for her fitness to pursue her Advanced Secondary Education.

**Age** …………… **Year** ………………… **Sex** …………………….

- **Blood count (Read and white)**……………………………………………………………
- **Stool Examination**………………………………………………………………………..
- **Syphilis and other veneral Diseases Test**………………………………………………..
- **T.B.** …………………………………………………………………..…………………………
- **Eye Test**………………………………………………...……………………………………..
- **Ears** …………………………………………………………..………………………..………
- **Spleen**………………………………………………………..…………………………………
- **Abdomen** …………………………………………………………………………………
- **Urine for protein test**…………………………………………………………………
- **Test for Pregnancy** ……………………..…………………..……………………………………

Additional information (If any) e.g. physical defects, impairment(s) e.g. arms, legs e.t.c, Infections chronic or family diseases etc

…………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………..

I certify that; the above student is fit /unfit to pursue her studies as required.

**Station** …………………………… **Signature and Official Stamp**……..…………………….………

**Date**……..…………………………… **Designation**……………………………………..…………

**<u>Note: Medical Officer</u>**

*At the time of examination please treat the individual for anything you note for student. This completed form should be sent to the school with your acceptance form brought when you come to school. No student can be enrolled without this certification physical fitness.*

---

## 6.0 (b) TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi ______________________________________

   Mahali alipozaliwa ___________________________________________

   Tarehe ya Kuzaliwa____________________ Umri___________________

   Anuani ya nyumbani ___________________________________________

   Shule ya Sekondari aliyosoma___________________________________

   Namba ya Mtihani Kidato cha Nne_______________________________

PICHA YA MWANAFUNZI

2. Jina kamili la Baba____________________________________________

   Kabila __________________________ Dhehebu ____________________

   Simu Na_________________________ Kazi.______________________

PICHA YA BABA

3. Jina kamili la mama____________________________________________

   Kabila ___________________________ Dhehebu ___________________

   Simu Na __________________________ Kazi ____________________

PICHA YA MAMA

4. Jina kamili la Mlezi ___________________________________________

   Kabila ___________________________ Dhehebu _________________

   Simu Na __________________________ Kazi ___________________

PICHA YA MLEZI *(Unaye ishi naye)*

5. Je, wewe unaishi na nani? Jina________________________________________________

   Uhusiano___________________________________________________________________

   Anuani ____________________________________________________________________

6. Je, uliwahi kuwa Kiongozi? Ndiyo/Hapana

   Kama ndiyo taja nafasi ilikuwa ipi?___________________________________________

   ___________________________________________________________________________

7. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo_______________________________________

   *(Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo, mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)*

## 6.0 (c) AHADI YA MZAZI/MLEZI

**Mimi (Jina kamili)**___________________________________________________________

Anuani ___________________________________________________________

Simu___________________________________________________________

Mzazi/Mlezi___________________________________________________________

Nakubali mtoto wangu (Jina lake) ________________________________________

1. Asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Lugalo, kadiri alivyopangiwa.

2. Nimempa fedha ya mahitaji inayotakiwa na nitashirikiana na walimu katika suala zima la malezi ya mwanangu na maendeleo yake kitaaluma na kumsaidia mtoto kufuata sheria za shule.

**Jina (Mzazi/Mlezi)**___________________________________________________________

Sahihi___________________________________________________________

Tarehe___________________________________________________________

Namba ya simu___________________________________________________________

Namba ya simu yenye **WhatsApp** ya kwako au miongoni mwa ndugu wa Mwanafunzi walioonyeshwa kwenye Fomu Hii (**ni Muhimu**) ______________________________

**Mimi (Jina la Mwanafunzi)**___________________________________________________________

Nimekubali nafasi hii, naahidi kufuata sheria za shule na kuwatii walezi , wakubwa na wanafunzi wenzangu, tena nitafanya bidii ya kujifunza ili nifaulu vyema masomo yangu .

Jina *(Majina Matatu)* ___________________________________________________________

Sahihi ___________________________________________________________

Tarehe ___________________________________________________________

## 7:0 OORODHA YA VITABU VYA MASOMO

Orodha ya vitabu vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anashauriwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa na **General studies** ni kwa wote.

### 7.1 PHYSICS

a) Muncaster,R.(1995). *A-Level Physics* ($4^{th}$ ed). Gluocestershire: Stanley Thornes (Publishers) Ltd, Delta Place: U.K(a) UP (University Physics)
b) Nelkon, M. & Parker, P. (1995). *A-Level Physics* ($7^{th}$ ed). London: Heinnemann Educational Books Ltd. London
c) Duncan. T (2000). *A-Level Physics ($5^{th}$ ed*). London: John Murray (Publishers). Ltd.
d) Mehta, R., & Mehta, V.K (2009). *Principles of Physics for Class XII*. New Delhi: S.Chand & Company Ltd.

### 7.2 ADVANCED MATHEMATICS

a) Backhouse, J.K & Houldsworth, S.P.T (1984). *Pure Mathematics Book 1*. Pearson Education Ltd.
b) Backhouse, J.K & Houldsworth, S.P.T & B.E.D Cooper (1985). *Pure Mathematics Book 2*. Longman Group Ltd.
c) Dass, H.K (2002). *Engineering Mathematics*. S.Chand & Sons Company Ltd.
d) Tranter, C.J & Lamb C.G. (1961). *Advanced Level Mathematics (Pure and Applied) $4^{th}$ Edition;* Hodder and Stoughton Educational Ltd.
e) Septine I. Sillem (2015). *Advanced Mathematics For Advanced Secondary Schools Form Five.* GDY Publications Ltd. DSM
f) Septine I. Sillem (2015). *Advanced Mathematics For Advanced Secondary Schools Form Six*. GDY Publications Ltd. DSM

### 7.3 GENERAL STUDIES

a) ZISTI KAMILI
b) Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012). *Understanding Advanced Level General Studies:* Advanced Level Secondary Schools,

### 7.4 CHEMISTRY

a) Ramsden
b) Schand ya V na VI
c) Schand Class XI na XII
d) Ann & Patrick-Advanced Chemistry

### 7.5 BIOLOGY

a) Biological Science (B.S)
b) Understanding Biology
c) Schand Class XI na XII